**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MTIHANI WA KUPIMA UMAHIRI KIDATO CHA SITA (FOSCE) -2025**

**CODE: 121/2** **KISWAHILI 2**

**MASAA: 3:00** **21 FEBRUARI 2025, ASUBUHI**

## MELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A na B yenye jumla ya maswali nane (8)
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali matatu (3) kutoka sehemu B swali la tano ni la lazima
3. Sehemu A ina alama 40 na sehemu B ina alama 60
4. Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali.
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa karatasi zako za kujibia.


*© FORM SIX COMPETENCE EXAMINATION (FOSCE) - 2025*

## SEHEMU A Alama 40

Jibu maswali yote

1. Fasihi ikitumiwa vibaya huweza kuleta athari hasi katika jamii. Ukiwa kama mwanafunzi wa kidato cha sita uliyobobea kusoma somo la Kiswahili shuleni kwako eleza athari tano za kutumia vibaya fasihi
2. Japokuwa fasihi ya Kiswahili ni kongwe lakini ni changa. Fafanua changamoto tatu zinazoikumba fasihi ya Kiswahili na njia mbili za kuondokana na changamoto hizo
3. Tofautisha maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kazi ya fasihi
   A. Mhusika kivuli na mhusika shinda
   B. Tanakali sauti na tanakali lafudhi
   C. Bumbwi na ramsa
   D. Hurafa na istiara
   E. Tenzi na tendi

4. Soma Makala ifuaatayo kisha chambua mbinu za kifani zilizotumika

Uwapi uzuri wako, haupo umepotea
Ya wapi malingo yako, na hashuo za dunia
Leo upo peke yako, sote tumekukimbia

Sasa ni chano cha maji, watu wajichanyatia
Umekwisha ujuaji, haya zimekupotea
Yale usiyotarajia, kwako yamekuhamia
Bao la mkahawani, kila mtu akalia
Juhaha huna usoni, na wala sitara pia
Wenyeji wote wa mjini, wamekwisha kupitia

Sasa jamvi la wageni, wajapo huwapokea
Imekutoka shamani, mtu duni mebakia
Hata mbwa wa mjini, kikuona hukimbia.


*© FORM SIX COMPETENCE EXAMINATION (FOSCE) - 2025*

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali 3 katika sehemu hii, swali la 5 ni la lazima

ORODHA YA VITABU

USHAIRI

| | |
|---|---|
| Kimbunga | H.G. Haji |
| Mapenzi bora | S.Robert |
| Chungu tamu | T.A.Mvungi |
| Fungate ya Uhuru | M.S.Khatib |

RIWAYA

| | |
|---|---|
| Usiku Utakapokwisha | M. Msokile |
| Kufikirisha | S. Robert |
| Mfadhili | H.I. Tuwa |
| Vuta N'kuvute | S.A. Shafii |

TAMTHILIYA

| | |
|---|---|
| Kwenye Ukingo wa Thim | E. Husein |
| Moran | E. Mbogo |
| Nguzo Mama | Penina Mhando |
| Kivuli Kinaishi | S. Mohamed |

5. Uteuzi wa taswira mbalimbali ni mbinu moja wapo inayotumiwa na wasanii kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Fafanua kwa mifano jinsi wasanii wa vitabu viwili vya ushairiulivyovisoma walivyotumia mbinu hiyo (hoja 4 kila kitabu)

6. Wasanii wa ushairi wana msaada endelevu unaochangia maendelea kwa jamii wanazo ziandikia. Toa hoja tatu (3) kwa kila diwani katika diwani mbili ulizosoma.

7. "Vijana sio watu wazuri". Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja nne kwa kila riwaya kutoka katika riwaya mbili ulizosoma

8. "Wasanii hutumia mitindo mbalimbali katika kutia ladha na kupevusha ujumbe uliopo katika kazi zao" kwa kutumia vitabu viwili (2) vya tamthiliya kati ya ulivyosoma onesha jinsi mitindo ilivyotumika kupevusha ujumbe uliomo. Toa hoja nne katika kila kitabu.


***© FORM SIX COMPETENCE EXAMINATION (FOSCE) - 2025***

*MWISHO*


***© FORM SIX COMPETENCE EXAMINATION (FOSCE) - 2025***